



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BENKI KUU YA TANZANIA



MPC NA.245

8 Oktoba 2026

Tamko la Kamati ya Sera ya Fedha

1. Riba ya Benki Kuu

Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ilikutana tarehe 7 Oktoba 2026 na kuamua Kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kubaki asilimia 6.25 kwa robo mwaka inayoishia Desemba 2026. Kiwango hiki cha Riba kitawezesha kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuwezesha ukuaji wa uchumi. Hivyo, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kubaki ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3 hadi 5.

Kutokana na ongezeko la bei za mafuta kufuatia mgogoro unaondelea Mashariki ya Kati na mvua El Niño zinazorajiwa nchini zinazoweza kuathiri bei za bidhaa mbalimbali, mwelekeo wa Sera ya Fedha unaweza kubadilika ili kukabiliana athari hizo. Aidha, hatua za kisera zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali katika kukabiliana na changamoto hizo zitawezesha kudhibiti mfumuko wa bei na kuendelea kuwezesha ukuaji wa uchumi.

2. Mwenendo wa uchumi wa dunia

Kamati ilitathmini mwenendo wa uchumi wa dunia na kuona kuwa mgogoro unaondelea Mashariki ya Kati umeathiri shughuli za kiuchumi na mnyororo wa ugavi wa mafuta na mbolea katika soko la dunia. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa bei za bidhaa mbalimbali hususan bei za mafuta na mbolea. Mathalan, bei ya mafuta katika soko la dunia imekuwa zaidi ya dola za Marekani 100 kwa pipa kwa siku za hivi karibuni.

Kutokana na hali hii, kasi ya ukuaji wa uchumi duniani inatarajiwa kupungua mwaka 2026, ikilinganishwa na mwaka uliopita. Shirika la fedha la Kimataifa (IMF) linakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia wa asilimia 3, kutoka asilimia 3.5, wakati Benki ya Dunia inakadiria ukuaji wa asilimia 2.5 kutoka asilimia 2.9. Mwelekeo huu wa uchumi wa dunia kwa kiasi kikubwa utategemea namna mgogoro wa Mashariki ya Kati utakavyoendelea.

Kutokana na kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia, mfumuko wa bei duniani umeongezeka. IMF wanakadiria mfumuko wa bei wa dunia kuwa zaidi ya asilimia 4 kwa mwaka 2026. Kutokana na hali hii, benki kuu za nchi nyingi zimesitisha utekelezaji wa sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi. Bei ya dhahabu imeendelea kuwa juu na inatarajiwa kuendelea kupanda. Mwenendo huu utaendelea kuongeza mapato ya fedha za kigeni nchini na akiba ya fedha za kigeni.

3. Mwenendo wa uchumi wa ndani

Kamati ilibaini kuwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar (OCGS) zimekamilisha zoezi la mapitio ya takwimu za Pato la Taifa kwa kuhuisha mwaka wa msingi *“GDP rebasing”* kwa Tanzania Bara na Zanzibar, mtawalia. Kwa upande wa Tanzania Bara, mwaka wa rejea *“Base year”* umebadilishwa kutoka mwaka 2015 hadi 2019, na hivyo kusababisha ongezeko la Pato la Taifa kwa mwaka 2025 kufikia Shilingi bilioni 234,104 (sawa na Dola za Marekani bilioni 92.3), kutoka Shilingi bilioni 230,073 (sawa na Dola za Marekani bilioni 90.7) kwa kutumia mwaka wa msingi uliopita. Kwa upande wa Zanzibar, Pato la Taifa limeongezeka hadi Shilingi bilioni 9,242 (sawa na Dola za Marekani bilioni 3.6), kutoka Shilingi bilioni 7,029 (sawa na Dola za Marekani bilioni 2.8). Aidha, taasisi hizo zilioanisha takwimu na hivyo kuwezesha uandaaji wa takwimu za Pato la Taifa na viashiria vingine vya kiuchumi kwa ngazi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kuzingatia takwimu zilizohuishwa, uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar uliendelea kuimarika na kukua kwa kasi kwa mwaka 2026. Uchumi wa Tanzania Bara ulikua kwa asilimia 6.0 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, na unakadiriwa kuzidi asilimia 6 katika robo ya pili na ya tatu, ukichangiwa zaidi na kuimarika kwa huduma za kifedha, uzalishaji viwandani, uwekezaji katika miundombinu na huduma za jamii. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi ulikua kwa asilimia 6.7 katika robo ya kwanza ya mwaka 2026, huku ukuaji ukikadiriwa kuzidi asilimia 7 katika robo ya pili na ya tatu. Ukuaji huo umechangiwa zaidi na shughuli za utalii, ujenzi na miradi ya umwagiliaji. Uchumi wa ndani unatarajiwa kuendelea kukua licha ya uwepo wa vihatarishi vinavyotokana na ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia, kuvurugika kwa minyororo ya ugavi na athari za mvua za El Niño.

Mfumuko wa bei kwa Tanzania Bara, umeendelea kubaki ndani ya wigo wa lengo la kitaifa wa asilimia 3 hadi 5, licha ya kuongezeka na kufikia asilimia 4.3 mwezi Agosti 2026, kutoka wastani wa asilimia 4.1 kwa robo mwaka inayoishia Juni 2026. Aidha, mfumuko wa bei umeendelea kuwa ndani ya vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Ongezeko hilo lilichangiwa zaidi na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, hali iliyosababisha kuongezeka kwa bei za nishati nchini na gharama za usafirishaji. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei ulipungua hadi asilimia 5.6 mwezi Agosti 2026 kutoka asilimia 6 mwezi Julai 2026. Hata hivyo, kiwango hicho kilikuwa juu ya wastani wa asilimia 5.5 katika robo mwaka iliyoishia Juni 2026, na lengo la muda wa kati la asilimia 5.

Hali ya ukwasi iliendelea kuakisi mahitaji ya shughuli za kiuchumi. Mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kuongezeka kwa kasi, kufikia wastani wa asilimia 32.5 katika robo mwaka iliyoishia Septemba 2026. Sekta ya kibenki iliendelea kuwa imara, ikichangiwa na uwepo wa mitaji, ukwasi wa kutosha, pamoja na faida. Mikopo chechefu ilifikia asilimia 2.5 mwezi Agosti 2026, kiwango ambacho ni chini ya ukomo unaohimilika wa asilimia 5. Wakati huohuo, mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi na uthabiti, huku idadi ya miamala ikiongezeka.

Sekta ya nje iliendelea kuwa tulivu licha ya kuongezeka kwa changamoto za migogoro ya kisiasa duniani. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka kidogo kutokana na athari za misukosuko ya kiuchumi ya nje na kufikia asilimia 2.5 ya Pato la Taifa katika mwaka ulioishia Septemba 2026, ikilinganishwa na asilimia 2.4 ya Pato la Taifa katika mwaka ulioishia Juni 2026. Hata hivyo, kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi hususan dhahabu, bidhaa za viwandani na huduma za utalii, kulisaidia kupunguza athari za kupanda kwa gharama za uagizaji wa bidhaa kutoka nje na gharama za usafirishaji. Kwa upande wa Zanzibar, urari wa malipo ya kawaida uliendelea kuwa na ziada, ukichangiwa zaidi na mapato yatokanayo na shughuli za utalii. Akiba ya fedha za kigeni iliendelea kuwa ya kutosha, zaidi ya dola za Marekani bilioni 6.0, yenye uwezo wa kugharamia uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi kwa miezi 4.3, juu ya lengo la kitaifa la angalau miezi 4.

Sera ya kibajeti iliendelea kuchagiza ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Mapato yatokanayo na kodi yalivuka malengo yaliyowekwa, huku matumizi ya Serikali yakiendelea kufanyika kuendana na rasilimali zilizopo, na hivyo kudhibiti nakisi ya bajeti, ambayo ilikuwa chini ya asilimia 3. Aidha, deni la umma liliendelea kuwa himilivu, huku deni la nje likichukua sehemu kubwa. Mikopo ya ndani iliendelea kuwa nyenzo muhimu katika kuongeza rasilimali zinazotumika kugharamia matumizi ya Serikali.

4. Tarehe ya kutangaza riba mpya ya Benki Kuu

Kamati itaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa mgogoro wa Mashariki ya Kati pamoja na vihatarishi vitakavyoambatana na mvua za El Niño na itachukua hatua stahiki za kisera kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unabakia ndani ya lengo.

Mkutano ujao wa Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) utafanyika tarehe 6 Januari 2027, na uamuzi kuhusu Kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kwa robo ya kwanza ya mwaka 2027 utatangazwa siku itakayofuata.



Emmanuel M. Tutuba

GAVANA